Wale wakoma wanne (4), walipofika kwenye kambi ya washami na kujiokotea utajiri kwa jinsi walivyoweza, biblia inatuonyesha baadaye dhamiri zao ziliwasuta, kwanini wanufaike wao peke yao, wakati Israeli nzima ipo kwenye janga kubwa la njaa?

Hivyo walipogundua ubinafsi wao, haraka sana bila kukawia walijirekebisha wakaenda kuwaambia wakuu wa Israeli, na baadaye watu wakaja kujikusanyia nyara kwa wingi kwa jinsi wawezavyo, na tangu huo wakati Israeli yote janga la njaa likapotea.

Watu wanne tu ambao hawakuwa wabinafsi, waliliokoa taifa zima,

2 Wafalme 7:3-11

> *[3]Basi walikuwapo watu wanne wenye ukoma, penye lango la mji; wakasemezana, Mbona tunakaa hapa hata tufe?*
>
> *[4]Tukisema, Tutaingia mjini, mjini mna njaa, nasi tutakufa humo; nasi tukikaa hapa, tutakufa vile vile. Haya! Twende tukaliendee jeshi la Washami; wakituhifadhi hai tutaishi; wakituua, tutakufa tu.*

*[5]Basi wakaondoka kabla ya mapambazuko, ili waende mpaka kituo cha Washami; na walipofika mwanzo wa kimo cha Washami, kumbe! Hapana mtu.*

*[6]Kwa maana Bwana alikuwa amewasikizisha Washami kishindo cha miendo ya magari, na kishindo cha farasi, kama kishindo cha jeshi kubwa; wakaambiana, Tazama, mfalme wa Israeli amewaajiri wafalme wa Wahiti, na wafalme wa Wamisri, waje wapigane nasi.*

*[7]Kwa hiyo wakaondoka, wakakimbia kungali giza bado, wakaziacha hema zao, na farasi zao, na punda zao, na kimo chao vile vile kama kilivyokuwa, wakakimbia wapate kujiponya nafsi zao.*

*[8]Basi wale wenye ukoma walipofika mwisho wa kituo, waliingia katika hema moja, wakala, na kunywa, wakachukua fedha, na dhahabu, na mavazi, wakaenda wakavificha; wakarudi, wakaingia katika hema ya pili, vile vile wakachukua vitu, wakaenda, wakavificha.*

*[9]Ndipo wakaambiana, MAMBO HAYA TUFANYAYO SI MEMA; leo ni siku ya habari njema, na sisi tunanyamaza; mkingoja hata kutakapopambazuka, madhara yatatupata; basi twende tukawaambie watu wa nyumba ya mfalme.*

> *[10]Basi wakaenda, wakawaita mabawabu wa mji; wakawaambia, Tulifika kituo cha Washami, na tazama, hapana mtu ye yote huko, wala sauti ya mtu, ila farasi wamefungwa, na punda wamefungwa, na hema zao kama walivyoziacha.*
>
> *[11]Na mabawabu wakaita wakawaambia watu wa nyumba ya mfalme.*

Hii inatoa sauti gani kwetu?

Sisi tuliookoka ni zaidi ya wanne.. Lakini kwanini injili haiwafikii wengi?  Ni kwasababu haya tuyafanyayo tunaona ni vema..

Tunaona ni sawa tu tuingie rahani mwa Mungu sisi wenyewe.

Ni sawa tu tuhubiriwe peke yetu, wengine waendelee kukaa nje ya kanisa..

Ni sawa tu tujazwe Roho, wengine waendelee kukaa chini ya vifungo vya mapepo.

Hii ni sifa ya ubinafsi.

Ikiwa upo kanisa, kila siku unahubiriwa lakini wewe huwahubirii wengine ni ubinafsi,

Ikiwa unafuatilia mafundisho kama haya mitandaoni, lakini wewe hutaki kushea na wengine, ni ubinafsi.

Ikiwa umeokoka muda mrefu, halafu huna tunda la mtu yeyote kuokoka kupitia wewe, ni ubinafsi..

Kujilimbikizia mambo ya ufalme peke yako…wenzako hawakishiriki kipawa chako, Si jambo jema linalokubalika kiroho

Nenda kahubiri.

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kubofya link hii >> https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10

Kwa mawasiliano: +255789001312 au +255693036618

Bwana akubariki.

Share on:
WhatsApp